

Tamko la Umoja wa Wanasaikolojia Duniani Juu ya Mchango wa Wanasaikolijia katika Maeneo yenye Migogoro ya Kimataifa.

Tamko hili, ambalo kwa mara ya kwanza lilitolewa na Chama cha Wanasaikolojia cha Marekani, (APA) mnamo tarehe 5 Juni, 2008 na likapitiwa na Umoja wa Wanasaikolojia Duniani (GPA) tarehe 31 Machi, 2022 linakusudiwa kuwatayarisha wanasaikolojia ili kutoa mchango unaofaa katika kukabiliana ipasavyo na majanga ya kibinadamu na kimaumbile.

Umoja wa Wanasaikolojia Duniani na Chama cha Wanasaikolojia cha Marekani inaunga mkono Kamati Kuu ya Pamoja (IASC) juu ya miongozo ya kusaidia afya ya akili na hulka za kijamii katika nyakati za dharura ya mwaka 2007. Lengo la miongozo hii ni kuwezesha kupanga na kuratibu msaada midogo midogo ya kibinadamu kutoka sekta nyingi (ambayo ni ya muhimu na ya kipaumbele kutekelezwa kwa haraka) ili kulinda na kuimarisha afya za akili ya watu na pia ustawi wa kitabia katika nyakati za hali ya dharura.

Miongozo ya kamati hizi iliandikwa kwa nchi za uchumi wa chini na uchumi wa kati, hata hivyo mfumo mzima unafanya kazi pia katika nyakati za dharura za nchi zilizoendelea. Wanasaikolojia ambao wamepata mafunzo katika kukabiliana na hali za dharura za kibinadamu au na za kimaumbile ambao pia hujumuishwa katika mashirika rasmi ya huduma za kibinadamu yenye mamlaka ya kupeleka wataalamu katika maeneo hayo pia wanalazimika kuifahamu miongozo hii.

Miongozo Ya Kamati Hizi inaelekeza kuwa:

- Mtu yeyote ambaye anatarajiwa kutoa huduma katika jumuiya za kimataifa, ikijumuisha wanasaikolojia, lazima awe anafanya kazi katika shirika la huduma za kibinadamu linalofahamika katika eneo la mzozo badala ya kuwa mtoa huduma anayejitegemea.
 - Mfano wa mashirika yanayojishughulisha na huduma za kibinadamu ni:

- Mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa kama vile Shirika la Kuwahudumia Watoto (UNICEF) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR).
- Mashirika ya Kimataifa Yasio ya Kiserikali kama vile Jumuiya ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu, Jumuiya ya Kimataifa ya Hilali Nyekundu, Jumuiya ya Kimataifa ya Madaktari na Madaktari Wasio na Mipaka.
- Wataalamu wote wa afya ya akili wa kigeni, ikijumuisha wanasaikolojia, ambao si sehemu ya shirika la huduma za kiutu **hawaruhusiwi** kwenda katika maeneo ya majanga isipokuwa watimize vigezo vifuatavyo:
 - Wawe wameshawahi kufanya kazi katika maeneo ya dharura ambayo ni sawa na yale ambayo wanakwenda wao wenyewe (hii ni kwa sababu maeneo ya vita na maeneo ya majanga ya kimaumbile yanahitaji mbinu tafauti na hayawezi kuchukuliwa kama dharura sawa, kwani kila aina ya mzozo unahitaji mafunzo maalumu).
 - Wawe wameshawahi kufanya kazi katika maeneo nje ya maeneo ambayo wamekulia na wawe wanafahamu tamaduni na lugha ya watu wanaokwenda kuwasaidia.
 - Wawe na uelewa wa msingi katika njia za kuingilia kati maeneo ya dharura kama ilivyoorodheshwa Katika Miongozo ya Kamati ya Pamoja.
 - Wawe na uelewa wa ama misingi ya afya ya umma au saikolojia (mtazamo wa) ya jamii
 - Wawe na mualiko wa kimaandishi kutoka taifa ambalo hali ya hatari imetokea au inatokea au wawe na mualiko kutoka shirika la kimataifa linalojulikana lenye mamlaka ya kutoka huduma katika maeneo ya hali ya hatari.
 - Wawe wameitwa kama sehemu ya shirika ambalo limeshamiriwa kuiweka jamii katika ustawi kwenye maeneo ya dharura.
 - Wasijielekeze kazi zao katika utekelezaji wa misaada yao (yaani kazi za kidakrari pekee) isipokuwa wawe tayari kutoa msaada kwa mpango mzima, ikiwemo kutoa elimu kwa wafanyakazi wazawa ili uingiliaji na misaada kama hiyo iwe inatekelezwa na wazawa” (IASC, 2007, uk. 74 – 75).

Kwa kuzingatia Miongozo ya Afya ya Akili na Msaada wa / Mwenendo asili wa Jamii zilizoko Katika Maeneo ya Dharura na jukumu la kimaadili ya kufanya kazi katika maeneo ambayo mtu anayamudu, (angalia IUPsyS Tamko la Pamoja la Maadili ya Wanasaikolojia, Kanuni Na. 2) inapendekezwa kuwa wanasaikolojia wanaotoka nje ya maeneo yanayohitajia dharura wasitoe misaada ya moja kwa moja katika nchi za kigeni na jamii zilizoathirika na maafa/majanga.

Kama vigezo vilivyotajwa hapa vimetimizwa, mwanasaikolojia anaweza kuchagua ILA (njia mbadala) juu ya sheria ya jumla. Mwanasaikolojia anayependa kusaidia katika juhudi za kiutu baada ya mizozo ya kibinadamu au ya kimaumbile anashauriwa kutafuta njia mbadala ambazo ni maalumu zinazoendana na katika kukabiliana na mahitaji ya shirika lililopo wakati huo.

Pale ambapo wanasaikolojia wataitwa kuchangia / kusaidia, inashauriwa kuwa msaada huo utakaotolewa uwe ni kwa utekelezaji wa ustawi wa kihulka ambapo mwanasaikolojia anaejitolea atoe ushauri na au mafunzo kwa wawezeshaji wakaazi.

Katika kutoa ushauri, mafunzo ya wakufunzi na pia vifaa vya harakati za uokozi / usaidizi kwa watu walioathirika na hali ya hatari, ni muhimu / lazima kwa wanasaikolojia kugundua / kujua / kutambua kwa undani / upeo / kwa upana mkubwa utofauti wa utamaduni na mtazamo wa kidunia juu ya nchi zao wenyewe, tamaduni, mila na muktadha wa jamii zilizoathirika. Wanasaikolojia wanaofanya kazi kusaidia watu katika maeneo yalioathirika na maafa lazima wawe na tahadhari na wawe na uelewa wa mitazamo na tamaduni tofauti katika kutoa mapendekezo. Kwa mfano, watu hawalingani kutoka eneo moja na jengine kwa namna wanayoyaona na kuyachukulia madhila yao kutokana na matendo mabaya wanayopitia. Vile vile, jambo la muhimu zaidi ni kuelewa kuwa njia na mbinu za kuponya majeraha / madhila hayo katika namna ambayo itaonekana ni sahihi na inafaa pia ni tofauti.

Mbinu mbalimbali za uponyaji / kuboresha afya ya akili zinahitaji uelewa na kufanya kazi pamoja na jamii husika pamoja na wahudumu / viongozi wa afya ya akili. Pia (mbinu hizo) zijumuishe makundi ya wahanga na mtu mmoja mmoja binafsi. Kuzitafsiri pekee dhana za kitaalamu (nyingi ni za kimagharibi kupandikizwa katika utamaduni fulani) na utoaji vifaa haitoshi. Matumizi mabaya za mbinu za utambuzi (wa matatizo ya kiafya) na hatua za matibabu bila ya kuwa na ushahidi / mifano /

vigezo juu ya jamii husika **unaweza kuwa na madhara** kwa walengwa (wale wanaokusudiwa kusaidiwa).

Tafiti na chunguzi lazima pia zielewe juu ya dhima ya kulinda maisha ya watu katika maeneo ya dharura. Hii itajumuisha miiko inayofaa na miongozo kwa ajili ya kulinda maisha ya watu (IASR Mapendekezo ya Uendeshaji wa Tafiti za Afya ya Akili za Kimaadili na Ustawi wa Jamii Zinazojali Mazingira ya Dharura, 2014).

Majukumu ya Wanasaikolojia Kimataifa

- **Kutoa Taarifa, Ushauri na / au Mafunzo kwa Wawezeshaji**
 - Wanasaikolojia wazoefu katika matatizo ya afya ya akili na au afya ya jamii wanaweza kusaidia katika kubadilishana uwezo unaofaa katika kurekebisha na kushauri kwa mashirika ya kuhudumia wanadamu au kutoa mafunzo kwa wenza wao kimataifa ili na wao waweze kuwawezesha wale wakaazi wa maeneo yao.
 - Hii huweza kufikiwa vyema kwa kufanya kazi na mashirika rasmi kama vile jumuiya ya kitaifa ya wanasaikolojia au jumuiya za kikanda / kieneo na jumuiya zisizokuwa za kiserikali (kwa mfano Jumuiya ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu au Jumuiya ya Hilali Nyekundu). Kama ombi la kutaka msaada limetoka katika jumuiya hizi, kuna uwezekano mkubwa ombi hili litakuwa limeratibiwa vyema kwenye taasisi rasmi na kuwekewa miundombinu imara ya utoaji misaada.
- **Kuandaa Mpango Jumuishi wa Utafiti Pamoja na Wanasaikolojia katika (ma)eneo yenye Migogoro**
 - Ushirikiano katikla tafiti utawasaidia wataalamu wa afya ya akili wa ndani katika kujifunza vipengele vya kiakili katika hali ya dharura, na kuweka misingi ya namna bora zaidi ya kukabiliana na hali hizo hapo baadae.
 - Makadirio bora ya mahitaji ya kiakili na vifaa na tathmini ya uingiliaji katika mazingira maalumu ni jambo la umuhimu wa kipekee.

Majukumu ya Wanasaikolojia Katika Nchi Zao

- **Kuwasiadia Watu Waliofikwa na Maafa Moja kwa Moja**

- o Wanasaoikolojia wanaweza kutafuta fursa katika jamii zao ili kuweza kutoa msaada kwa watu ambao wameathirika moja kwa moja kwenye majanga ya kibinadamu au ya kimaumbile.
 - Hii huweza kuwajumuisha watu kutoka maeneo yalioathirika na au wale ambao wapendwa wao/jamaa zao wameathirika.
 - Pia huweza kujumuisha wafanyakazi wa kutoa misaada wa kimataifa ambao wamesharudi nyumbani.

- **Kutangaza Miongozo Na Viwango Vya Kimataifa**

- o Wanasaoikolojia wanaweza kujisomea kuhusu namna ya kushughulika ustawi wa jamii kimataifa na vile vile kusambaza taarifa za viwango na miongozo ya kimataifa. Hii itasaidia kuhakikisha usaidizi unakuwa sahihi na kwa utaratibu maalumu.

- **Kutangaza Uelewa Juu ya Utofauti wa Kitamaduni Wakati wa Kusaidia Uponyaji wa Mateso, Uingiliaji Unaofaa na Mikakati ya Usaidizi wa Matatizo ya Kiakili.**

- o Msongo wa mawazo, namna ya kusaidia hali hiyo na njia bora na sahihi za uponyaji haya yote yaendane na tamaduni za jamii husika. Usaidizi/uingiliaji wa kimataifa sio tu jambo la kuzitafsiri na kutumia mikakati kutoka nchi nyengine; ila kila njia na uingiliaji wote kwa ujumla lazima uendane na mazungumzo pamoja na jamii hiyo na wataalamu wazawa na ujengwe katika muundo wa ushirikiano endelevu.
- o Wanasaoikolojia lazima waelewe kuhusu tamaduni, imani, lugha na utofauti wa kieneo, kisiasa na kijamii, ambao huu ndio hufanya mazingira kamili ya uokoaji, usimamizi na upatikanaji wa misaada kwa wazawa na mchango wa wazawa kwa jamii zilizoathiriwa. Wanasaoikolojia lazima waingize kipengele hiki katika mafunzo na ushauri wao.

Kujitayarisha kwa Ajili ya Baadae

Wanasaikolojia wanaotaka kujitolea katika maeneo ya usaidizi wanapaswa kujitayarisha sasa kwa kupata mafunzo ya kuhudumia maafa ya afya ya akili. Mahitaji ya muda mrefu kwa wataalamu wabobezi wa ushauri na mafunzo katika maeneo ya maafa yataendelea kuhitajika kwa muda mrefu ujao.

Matarajio ya Kutokea Madhara

Ni jambo la msingi kwa mwanasaikolojia kujielekeza msaada wake katika upeo wa eneo lake la kitaaluma. Kufanya vyenginevyo huweza kusababisha madhara kwa msaidiwa ambayo ni ukiukaji wa miiko / maadili ya kazi yake. Jukumu la mwanasaikolojia kutambua mipaka ya utendaji wake ni muhimu sana hasa wakati wa kufanya kazi na watu walio katika mazingira magumu kabisa kama vile watu wenye kiwewe / msongo wa mawazo (PTSD). Kupata dalili za tatizo kunatofautiana kulingana na mazingira ya kijamii na kitamaduni. Hivyo hivyo, njia za kuyaendea / kuyatibu matatizo hayo pia hutafautiana. Kushindwa kukabilana na hali hizi au majaribio ya kutaka kusaidia ambayo hayaendani na tamaduni husika huweza kuifanya hali kuwa mbaya zaidi na matokeo ya kutisha huweza kupatikana.